**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI MAJI YA CHAI**

S.L.P. 11061
**ARUSHA**

Kumb. Na: MCSS/J.I/VOL.1/21

20th MAY, 2021

Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi
...................................................
S.L.P....................................
.............................................

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAJI YA CHAI HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU MKOA WA ARUSHA KIDATO CHA TANO MWAKA 2021**

1.0 Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha TANO katika Shule hii mwaka 2021 Shule hii ipo katika Kata ya Maji ya Chai, Wilaya ya Arumeru, Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Mkoani Arusha mbele kidogo ya Mji mdogo wa Maji ya Chai, barabara Kuu ya Arusha – Moshi kituo cha Njia ya Ng'ombe, kilomita 1.5 kutoka barabara kuu.

2.0 Amechaguliwa tahasusi ya (i) HGL ( )(ii) HKL ( ) (iii) PCM ( )

3.0 Shule hii ilianzishwa mwaka 1998, na ina kidato cha 1 hadi cha 6. Kidato cha I – 4 ni wanafunzi wa kutwa bali kidato cha 5 – 6 ni wa Bweni **Wavulana tu.**

4.0 Muhula wa masomo unaanza tarehe 05/07/2021 mwisho kuripoti ni tarehe 20/07/2021 Saa kumi na moja na nusu jioni. Mwanafunzi ambaye hataripoti ndani ya tarehe zilizotajwa atahesabiwa kuwa ameikataa nafasi hiyo.

5.0 **MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA**

5.1 **KARO YA SHULE (SCHOOL FEES)**

(i) Ada ya Shule kwa mwaka ni Shs.70, 000/= kwa mwanafunzi.Unaweza kulipa kiasi cha Tshs.35,000/= kwa muhula, au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hiyo ilipwe kwenye akaunti namba 40801200281,NMB Jina Maji ya Chai Sec. Recurrent.
(ii) Tahadhari(caution money) sh.5,000/= fedha hii haitarejeshwa.
(iii) Wapishi, walinzi na vibarua wengine shilingi 30,000/=
(iv) Picha/kitambulisho shilingi. 6,000/=
(v) Taaluma shilingi 20,000/= kwa muhula; hivyo kwa mwaka ni shilingi 40,000/=

(vi) Nembo ya shule shilingi. 2,000/=

(vii) Mkutubi shilingi 10,000/=

(viii) Huduma ya kwanza shilingi 10,000/=

(ix) Ukarabati wa Samani shilingi 15,000/=

Fedha zote zilipwe kwenye akaunti hiyo hiyo ya Shule namba 40801200281 NMB. Jina la akaunti ni Maji ya chai Sec.Recurrent( Andika jina kamili la mwanafunzi kwenye pay in slip) Iwapo wewe unafadhiliwa na Serikali kuu, Halmashauri au Shirika/Taasisi yeyote huna budi kuwasilisha Hundi au uthibitisho rasmi kabla ya kupokelewa/kusajiliwa.

5.2 **SARE YA SHULE (SCHOOL UNIFORM)**

(i) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi ya tetroni

(ii) Suruali mbili (2) za kitambaa rangi ya kijivu(Ash gray) upana wa suruali kwa chini ni sentimeta 16 na iwe na marinda mawili kwa kila upande

(iii) Sweta moja (1) la kijivu

(iv) Tai moja (1) ya kijivu yenye miraba myeupe

Aidha mwanafunzi anashauriwa kuja kujishonea sare yake afikapo Arusha kuepuka hasara na mkanganyiko wa rangi za sare ya shule uliojitokeza mwaka jana na kupelekea kila mwanafunzi kuja na sare yake tofauti shuleni iliyosababisha kurudia kushona sare halisi ya shule.

v)Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vinavyopigwa rangi na visiwe na visigino virefu (highhill)

vi)Soksi nyeusi jozi mbili (2)

NB. **Hairuhusiwi kuibana suruali kuwa mnyonyo au kuvaa mlegezo awapo shuleni.**

5.2.3 **MAHITAJI YA MALAZI YA BWENI.**

(i) Godoro moja (1) la sponji lenye upana wa futi mbili na nusu.

(ii) Shuka mbili za rangi ya light blue.

(iii) Blanketi moja.

(iv) Nguo za kulalia (night dress) na taulo.

(v) Sanduku imara la kuhifadhia mali yako. Tafadhali liwe moja la chuma lenye kufuli

(vi) Mahitaji yote ya usafi binafsi mf. sabuni, mafuta ya kujipaka,mswaki na dawa ya meno.

(vii) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.

(viii) Sweta au koti lenye staha na lisilo na kofia na urefu usiovuka kiuno. Litavaliwa wakati wa kujisomea usiku.

(ix) Kila mwanafunzi awe na T-shirt za njano mbili zisizo na **MAANDISHI YOYOTE** na suruali nyeusi mbili za kitambaa kwa ajili ya kazi za nje hasa baada ya masomo. Epuka kununua jezi za timu mbalimbali au jeans/cadeti kama mbadala wa shamba dress. **(Vyote hivyo lazima mwanafunzi aje navyo).**

**5.2.3 VIFAA KWA AJILI YA CHAKULA.**

(i) Sahani moja

(ii) Bakuli moja

(iii) Kijiko kimoja

(iv) Kikombe kimoja **(mwanafunzi aje navyo).**

5.2.4 **VIFAA VYA MICHEZO**

(i) Bukta ya rangi nyeusi
(ii) T-shirt nyekundu – isiyo na maandishi
(iii) Raba za michezo jozi 1
(iv) Soksi nyeusi jozi mbili

N.B: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za aina nyingine tofauti na zilizotajwa katika fomu hii.

5.2.5. **MAHITAJI MENGINE:**

(i) Mfuko mzuri wa kubebea vifaa vya masomo.
(ii) Chandarua
(iii) Madaftari makubwa (counter books)yasiyo pungua matano kwa ajili ya masomo.
(iv) **Rimu mbili za karatasi**, moja ya mistari (**ruled**) na nyingine $A_4$ aina ya NOPA kwa ajili ya mitihani ya ndani.
(v) Mathematical Instrument (vifaa vya hesabu) kwa wale wa HGL na PCM tu.
(vi) **'Scientific Calculator'** kwa PCM na HGL.
(vii) Vitabu vya ziada masomo husika.
(viii) Brashi ya kusugulia chooni moja ,ufagio wa chelewa mkubwa yenye mpini kwa kila mmoja( For All Combinations).
**(ix)** Wale wa HGL kila mmoja aje na moper na ndoo yake.na HKL –Kila mmoja aje na Reki; PCM – Kila mmoja aje na jembe lenye mpini.
**(x) JUMLA YA FEDHA ZINAZOTAKIWA KULIPWA SHULENI KWA MWAKA NI T.SHS: 188,000/=**
**MUHULA WA KWANZA NI: T.SHS.133,000/=**
**NA MUHULA WA PILI NI T.SHS: 55,000/=**

Mwanafunzi atasajiliwa endapo atakuwa amezingatia na kutimiza maelekezo yote yaliyoainishwa kwenye fomu hii. Zingatia kuepuka usumbufu.
Mwanafunzi atatakiwa kurudisha fomu hii ikiwa imejazwa kikamilifu.

..........................
**KASANDA J.T**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
MAJI YA CHAI SEKONDARI
S. L. P 11061
ARUSHA

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

**SEHEMU A.**
**IJAZWE NA MWANAFUNZI.**

1. Jina kamili la mwanafunzi ---------------------------------------------------------------
2. Tarehe ya kuzaliwa ------------------------------------------ Dini ----------------------
3. Mahali alipozaliwa (kijiji) --------------------------- Kata -------------------------
4. Tarafa --------------------------------------------- Wilaya -----------------------------------
5. Shule alipomalizia kidato cha nne (4) ------------------------------------------------
6. Umewahi kuwa kiongozi shuleni 1. ---------------------------------------------------
7. Michezo unayopendelea ------------------------------------------------------------

**SEHEMU B.**
**IJAZWE NA MZAZI.**

1. Jina la Mzazi/mlezi --------------------------------------------------------- Simu ----------
2. Kazi na anwani ya mzazi/mlezi ------------------------------------------------------------
3. Mtoto anaishi na -----------------------------------
4. i. Dini ya Baba ------------------------------------------------- Dhehebu ---------------------
   ii. Dini ya mama --------------------------------------------- dhehebu ----------------------
   iii. Dini ya mtoto -------------------------------------------- dhehebu ----------------------

Anwani kamili ya nyumba ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo……………………………………………………………………………..

Mimi --------------------------------------------------------------Baba/mama/mlezi wa ------------------------------------------------ nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na uongozi wa shule kujenga nidhamu,taaluma, juhudi na maarifa kwa mwanangu katika kuitikia wito wake kielimu.

Tarehe ---------------------------------------------------------- Saini ------------------------------------

**SEHEMU C.**
**IJAZWE NA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI / SERIKALI YA MTAA**

Mimi ------------------------------------------------- ninathibitisha kuwa Ndg. --------------------- ------------------------------------------- ni mzazi/mlezi wa ------------------------------------------ na taarifa za mtoto na mzazi/mlezi ni ------------------------------ saini -------------------------

Naahidi kutoa ushirikiano wa kila namna pindi tatizo linapotokea kwa muda wote kijana awapo shuleni

Saini na Mhuri wa Afisa Mtendaji ------------------------------------------

Tarehe --------------------------------

**MUHIMU**

**AJE NA CHETI CHA MATOKEO YA KIDATO CHA NNE (RESULT SLIP) NA CHETI CHA KUZALIWA (COPY)**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NASERIKALI ZA MITAA**

A. **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu No. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara zenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili,"mf. asifuge kucha, ndevu, na nywele ndefu", mavazi na mazingira ya shule yawe safi muda wote.
(g) Kuvaa sare kamili ya shule wakati wote unapotakiwa (No outfits that are tight,short,or transparent are allowed.Shorts only allowed for games).
(h) Kuwepo kwa wakati sehemu zote anazohitajika na kuzingatia ratiba ya shule kama ilivyoelekezwa.

B. **MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.**

1. Wizi wa mali ya shule au ya mwenzake
2. Uasherati/ uzinzi/ulawiti/ubakaji na ushoga
3. Ulevi wa aina yoyote (pombe na aina zingine zote za madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, kuberi, sigara n.k.
4. Kupiga au kupigana na mwanafunzi au mwalimu/mtumishi wa shule.
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule au ya mwenzake
6. Kudharau Bendera ya Taifa
7. Kuoa au kusababisha mimba.
8. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo, kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
9. Kukataa adhabu kwa makusudi.
10. Kukutwa nje ya shule pasipo ruhusa maalumu kutoka uongozi wa shule
11. Kukutwa au kumilika simu ya mkononi au vifaa vyake mf. line, charger, betri ya simu.
12. Kulala nje ya Shule pasipo ruhusa maalumu kutoka uongozi wa Shule.
13. Kukutwa sehemu zifuatazo: -
    (a) Makazi/nyumba za watumishi wa shule hii bila ruhusa.
    (b) Kumbi za starehe na burudani.
    (c) Vilabu vya pombe

13. Utoro wa siku 90 bila taarifa.
14. Kutoa lugha chafu ya matusi kwa wanafunzi, walimu na watumishi wengine.
15. Kufuga ndevu na nywele (wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni).

Baada ya kusoma na kuielewa vizuri sehemu hii, mzazi/mlezi na mtoto wake watatakiwa kusaini ikiwa ni kuahidi kutoa ushirikiano wa kutosha.

SAHIHI YA MWANAFUNZI..........................SAHIHI YA MZAZI/MLEZI................

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**MAJI YA CHAI SECONDARY SCHOOL**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.**

To be completed by Medical Officer in a Government Hospital in respect of all new entrants to Maji ya Chai Secondary School ARUSHA.

Full name ------------------------------------------------------------------------------------
Age: -----------------------------------------------------------------------------------------

1. "AIDS' Test ---------------------------------------------------------------------------
2. Blood count (red & white) --------------------------------------------------------
3. Urine examination ------------------------------------------------------------------
4. Stool examination ------------------------------------------------------------------
5. Syphilis test ------------------------------------------------------------------------
6. T.B Test -----------------------------------------------------------------------------
7. Ear Test ------------------------------------------------------------------------------
8. Eye Test ------------------------------------------------------------------------------
9. Spleen Test --------------------------------------------------------------------------------
10. Abdomen Test---------------------------------------------------------------------------------
11. Additional information or any other physical, mental, hereditary or intoxication diseases.
    ----------------------------------------------------------------------------------------------
    ----------------------------------------------------------------------------------------------
    (Please state nature of treatment)
    .....................................................................................................................
    ...................................................................................................
    I certify that the above mentioned has been examined and found it to/ not to pursue further education.
    Signature ------------------------------------------
    Designation ------------------------------------------
    Station ----------------------------------------------

    Date: ---------------------------------------------------------
    Official stamp ----------------------------------------------